

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION
(CKRC)**

VERBATIM REPORT OF

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,
LUGARI CONSTITUENCY, AT
FRIENDS CHURCH LUMAKANDA.**

29TH JULY 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS – LUGARI CONSTITUENCY
AT FRIENDS CHURCH LUMAKANDA ON 29TH JULY 2002.**

Present:

Com. Abida Ali – Aroni
Com. Domiziano Ratanya
Com. Keriako Tobiko

Secretariat staff in attendance:

Ismael Aden
Mercy Mayabi
Susanne Motile

The meeting started at 10.05 a.m. with introduction by the Coordinator Mr. Amaswache Caleb Temba and prayers by Ms. Ambane, with Com. Abida Ali – Aroni in the chair.

District Coordinator, Mr. Temba: Wananchi watukufu, maCommissioners kutoka katika tume ya Katiba ya Kenya marafiki wote wenye wako hapa hamjamboni nyote? Kabla hatujaanza mkutano tutamwomba dada yet miss. Ambane atupe maombi halafu tuanze mkutano.

Ms. Ambane: Na tuombe; Eeh Baba Mwenyezi Mungu tunakushukuru kwa siku ya leo kwa kutwezesha kufika katika kikao hiki cha leo. Baba, tumekuja kuzungumzia yale yatakuwa na manufaa katika nchi yetu ya Kenya na vizazi vijavyo. Baba tunakuomba mwanzo mwema na mwisho mwema. Kwa jina la Yesu Kristo ninaomba. Amen.

Mr. Temba: Kabla hatujaanza, nitainroduce committee members wa Lugari CCC wenye wako hapa, na kwa saa hivi naona ni wawili peke yao. Mr. Timothy Akaranga huyo ndiye secretary wetu, Miss Ambane please say hi to everybody.

Ms. Ambane: Secretary, wananchi, hamjambo, hamjambo tena? Ahsante.

Mr. Temba: With us Commissioners today, is the District Secretary KNUT, Mr. Nyambira. Please welcome.

Mr. Nyambira: Hatutaenda kwa maneno mengi, kwa sababu tunajua watu wako njiani wanakuja na wale wamekuja mbeleni lazima wahudumiwe kwanza. Hapo katika advertisement ile tulisema we shall serve on the first come first served basis, kwa hivyo wenye watakuja-memorandum niuazo ni nataka tuanze mkutano. I am handing over the meeting to the Commissioners. Thank you very much.

Com. Aroni: Asante sana Bwana co-ordinator. Kwa niaba ya Tume ya Marekebisho ya Katiba tungependa kuwakaribisha katika hichi kikao cha leo na kuwaeleza kwamba huu ni mkutano rasmi wa upande huu kwa kutuwezesha kuchukua maoni yenu. Kabla sijasema mambo mengi, ningependa kuwajulisha kwa wanatume ambao wako hapa, pamoja na wenzetu ambao tumeandamana nao kutoka katika kikao cha Commission kule Nairobi, na ningeanza kwa kuwajulisha Commissioner Domiziano Ratanya na kumwomba awasalimie.

Com. Ratanya: Hamjamboni nyinyi nyote wananchi? Jina langu ni Commissioner Ratanya.

Com. Aroni: Mwenzangu mwingine ni Commissioner Keriako Tobiko.

Com. Tobiko: Hamjambo watu wa Lugari. Jina langu ni Tobiko, Commissioner.

Com. Aroni: Baada ya kuwajulisha kwa maCommissioners, ningetaka kuwajulisha wenzetu wengine. Kwanza kabisa, tunaye Bwana Ismael Aden ambaye ni Programme Officer na ndiye atakayekuwa anasimamia mipango ya kazi hii ya leo, na mkiwa na mazungumzo au maswali yoyote mnaweza kuzungumza naye. Halafu tuna msaidizi wa Bwana Aden, -Assistant Programme Office, ambaye ni Mercy Mayabi. Mercy atakuwa anaandika mambo yenu. Halafu, tuna verbatim recorder ambaye atakuwa ananasa sauti zenu na jina lake ni Suzanne Mutile. Na mimi, naitwa Abida Ali - Aroni, Naibu wa Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Katiba, kwa hivyo sote tunawakaribisha.

Kabla hatujaanza mkutano wa leo tungetaka kuwapatia masharti ambayo tunataka kuyafuata katika utaratibu wa siku ya leo. Kwanza kabisa tunawaomba nyote mjiandikishe katika meza ambayo iko pale nje, na hapo utasema ikiwa unataka kuzungumza au una maandishi ambayo ungependa kutoa, au pia ikiwa umekuja tu kusikiza, tafadhali utasema pale nje. Tungetaka kujua ni watu wangapi wamefika katika mkutano wa leo. Kwa hivyo hata ikiwa hauzungumzi tafadhali jandikishe pale nje.

Kuhusiana na mambo ya kujiandikisha, tungependa kuwaeleza kama mlivyoielezwa na Bwana Co-ordinator, tutawaita kulingana na jinsi ambavyo mmefika na kukiandikisha na tunawaomba msijaribu kutuuliza kuruka kwa sababu tunasema first come first served na tungependa sana kufuata utaratibu huo. Kwa hivyo, ikiwa kuna mtu amechelewa asijaribu kuomba kuruka utaratibu ambao tumeuweka.

Sasa katika mambo ya kuzungumza, mnaweza kutumia lugha yoyote ambayo mnadhania itaeleweka sawasawa. Lakini ikiwa unaweza kuzungumza Kiingereza au Kiswahili tutakuomba sana uzungumze hizo lugha mbili ili tuweze kukuelewa bila mtu yeyote kututafsiria kwa sababu tunajua katika tafsiri kuna mambo mengine ambayo huwa yanapotea. Lakini ikiwa huwezi, utatueleza-nina uhakika Bwana Co-ordinator ameweza kutuwekea mtu atakayeweza kutafsiria kwa lugha ambayo wanatume wataweza kuelewa.

Kwa watu ambao wana written memorandum, tutawapatia dakika tatu ya kuweza kutosomea muhtasari kwa kifupi kwa sababu tutapata nafasi ya kuweza kusoma hizo nakala baada ya kikao hiki. Tunajua ya kwamba mtajitokeza kwa wingi ndio maana hatutaki kukupatia nafasi ya kusoma kwa sababu tungetaka kila mtu ambaye amefika hapa, ikifikia saa kumi na moja awe amemaliza, tumewamaliza nyote.

Ambao watakuwa wanazungumza, tutawapatia dakika nne peke yake na baada ya kuzungumza ikiwa kuna mambo hatukuelewa, tunaweza kuuliza maswali ili tuweze kuelewa mazungumzo yenu zaidi. Na ikiwa pengine hauna jibu utatueleza. Ikiwa una jibu kuhusu swali ambayo tunawauliza, basi unaweza kujibu.

Baada ya kuzungumza, tuna register ambayo iko hapa kule ambako Ismael ameketi, na utakwenda na kujiandikisha. Kuna entries fulani ambazo ni lazima tuzipate na atakupatia nafasi ya kuweza kujaza hizo entries.

Na jambo lingine ambalo tunaomba sana, ni kwamba mtu akifika pale mbele na kuzungumza, ajaribu sana kutumia microphone kwa sababu tumewaeleza tunanasa sauti zenu kwa sababu hatutaki kubakisha jambo lolote. Kwa hivyo tuna watu karibu watano wanaandika, lakini tunataka kunasa hizo sauti kupitia chombo ambacho kiko hapa mbele.

Na jambo lingine ni kwamba, tunawaomba mtu akizungumza, ikiwa haufurahii maneno yake tafadhali usinung'unike au kupiga kelele, tumpatie nafasi amalize kusoma kwa sababu na wewe utapata nafasi ya kuja na kupendekeza. Tumeelewana?

Basi tunawashukuru sana na kufikia wakati huu, tungependa kuanza na Bwana Brown Ombugo. Tafadhali keti pale na ukimaliza - use the mic and stand - you are free to stand or sit.

Bwana Ombugo: Macommissiner ambao mmefika hapa leo, mimi yangu nitasema kwa kiswahili na pale nitashindwa nitaongea kwa Kizungu. Basi, mimi naitwa Brown Ombugo, mimi ni mwenyeji wa Lumatanda. Ninaenda kwa utaratibu wenu wa kitabu hiki.

Uraia - nitaanza na uraia: Wananchi wetu wa Kenya tuna shida sana kwa upande wa kupata uraia ambapo inakubidi lazima ulipe pesa fulani ili upate kitambulisho na neno hilo lazima litolewe.

Vitambulisho vipeanwe bila masharti yoyote hasa kwa mwananchi ambaye ni Mkenya - yule babake in Mkenya na mama ni Mkenya. Lakini kwa wale ambao mama ni wageni, sioni ni taabu. Mama akiwa ndiye Mkenya na baba ndiye Mzungu au kabila nyingine, basi huyo ni nafikiri tutakuwa na tashwishwi. Lakini so long as one of the parents is a Kenyan, definitely this person qualifies to be a Kenyan and he must be given an I.D free of charge.

Kwa pointi ya pili ambayo naambiwa mambo ya ulinzi wa taifa, kuna vyombo vya ulinzi. I would like to say ya kwamba,

Wakuu wa Kijeshi wateuliwe au wawe proposed by the President but they must be appointed by the Parliament. This will allow us to have the President not misusing them, ama wasiwe katika hali ile ya kutumiwa na chama fulani ambacho kiko namlakani. Wakuu wa jeshi wateuliwe tu by - they should be proposed by the President and then the appointment should be made by the Parliament. The same to the police forces, GSU, Wakubwa wa Jela na wengine wote. All the armed forces, the Heads, must be appointed by the Parliament and not the President. Because the President tries to misuse these people at his own whims and appoints people on tribal balance basis.

Kwa upande wa vyama vya kisiasa, ni nafikiri hapo tunaweza kuwa na vyama vingi vile Wakenya wanataka. Hata ikiwa kila mtu atakuwa na chama, hiyo ni shauri yao. Lakini, for finances, I think the Government should ensure that in their budget, they have some money for these political parties. So each and every registered party must at least get a small share of its money from the Government.

Now muundo na aina ya serikali: Nafikiri serikali yetu iwe ya kidemokrasia whereby the people must elect the President directly and also the VP. The VP must not be appointed by the President. Because then he serves as an Assistant Minister - he has nothing to say. Take a case of the current Vice President, he cannot tour anywhere, he cannot say anything - hawezi sema chochote maana boss yake atamfuta. Lakini ikiwa sisi ndio tutamteua huyu mtu au tutamchagua through ballot nafikiri atakuwa na nguvu na anaweza kukataa yale Rais atakuwa anamwambia.

Na tusiwe na Prime Minister. Sioni haja ya kuwa na Prime Minister katika hali hiyo. Mambo ya waziri mkuu, nafikiri hakuna haja tuwe tu na Rais na Makamu wa Rais ambao watachaguliwa na wananchi wenyewe.

Kwa upande wa Bunge, kitu cha kwanza, Mbunge lazima awe na umri usio chini ya miaka 25, awe ni mtu ambaye amesoma hadi kidato cha nne na awe ni mtu ambaye ana sifa njema. Asiwe amewai kuwa mwizi ama ametajwa katika tume yoyote ya wizi. We have had Parliamentarians who have done wrong and are just picked because they have the money - ni watu ambao wanavyo kwa hivyo wananunua kura za wananchi ambao ni maskini.

Asiwe mtu ambaye amewahi kufanya kazi ambayo ilikuwa inampatia pesa nyingi kuliko zile atapata kwa Bunge. Kwa hivyo mtu kama huyo itambidi in order to meet his more expenses here and there he will definitely poke his nose into the wrong place.

Kwa hivyo, kwa upande huo, nafikiri wajumbe wetu watakuwa ni watu walio tabia njema na wananchi ndio wataamua.

Katika upande wa kuchaguliwa, nafikiri tuna shida ambapo serikali inajaribu kuingilia uchaguzi. Neno hili nafikiri lingekuwa bora ikiwa Rais anayetawala, wakati analivunja Bunge naye pia “avunjwe” aende nyumbani, ili serikali iachwe katika mamlaka ya Chief Justice. Kukiwa na mtu wa aina hiyo, Chief Justice ama mteule wa kikanisa, a church leader, ashikilie serikali hadi wakati tunafanya uchaguzi na ili Rais mgeni aweze kuja. Rais anayekalia huwa anajaribu - he tries to interfere with election and only those he favours will always be his men in the Parliament.

Com. Aroni: Mr. Ombugo please your time is up. I will give you a minute to summarize.

Mr. Ombugo: But I think you are here, the whole day?

Com. Aroni: I will give you one minute to summarize, because we have over 50 people at the moment waiting to be heard. Tafadhali tuheshimu sheria ya mkutano.

Mr. Ombugo: Katika upande wa mamlaka ya Courts, the Chief Justice, Judges and Magistrates and so on, lazima wateuliwe na Parliament, wasiwe wa kuteuliwa na Rais. Rais anajaribu na kuwatumia vibaya.

Halafu mwishowe, Auditor General awe ni mtu ambaye ameteuliwa na Bunge. Asiwe ni mtu wa kuteuliwa na Rais. Maana hapa, Rais anajaribu kumtumia katika njia mbaya. Kwa hivyo, Auditor General awe ni mtu ambaye hajateuliwa na Rais.

Halafu, kwa upande wa mali ya asili yetu. Nafikiri hapa watu wetu wanavitumia vibaya. Mtu ana mashamba karibu acre 500 na bado ananyemelea forests zetu! Kwa hivyo lazima tufanye hivi: The biggest size of land somebody should have in Kenya should be 50 acres, not more than that. Ili, wale wanyakuzi waweze kurudishwa chini. Na wananchi wapewe mamlaka: ikiwa kuna mtu ana acre 500 ama elfu mbili, wavamie shamba hilo na wamwachie acre 50. Kuna watu humu wana acre 300 na wengine hawana chochote. Wananchi wapewe mamlaka na Tume hii, ili wavamie shamba lile, wamwachie acre zake hamsini na hizi zingine zichukuliwe. Ahsante.

Com. Aroni: Ahsante sana Bwana Ombugo, jilandikishe hapa na kutuachia memorandum ili tusome maelezo mengine ambayo hukuyazungumza. Ahsante sana. Next Simon Agona. I will give you 3 minutes to summarize your memorandum please.

Mr. Agona: Ahsante. Jina langu mimi ni Simon Agona Kigasia, ninatoka kule Mautuma location. Nitaanza hivi:

Com. Aroni: Tafadhali tusizungumze tukiwa hapa - tunanaza sauti, na tutakosa kusikia sauti ya Bwana Simon. Please, you can speak outside if you must. Thank you.

Mr. Agona: Nataka kuanza hivi: Ili Katiba iwe nzuri, lazima iwe na utangulizi. Kwa hivyo, nakubaliana na kwamba tuwe na preamble inayosema Katiba ni ya kina nani, na ni ya watu gani, na ni kwa sababu gani imeundwa. Kwa hivyo tunahitaji utangulizi.

Citizenship: Kuna vitambulisho vingi ambavyo tunavyo, vinavyotutambulisha kama wananchi. Ningependa vile vitambulisho vyote viwe katika kitambulisho kimoja. Ninamaanisha kwamba tuna I.D Card, passport, tuna ile ya kura, tuna zile zingine

tunapata hata hospitali, mbona kitambulisho kisiwe tu kimoja kile kinaweza kunasa mambo yote ya Mkenya halisi.

Upande wa Provincial Administration: Ile structure tunayo saa hizi, tunahitaji iwe trimmed ili tuwe na - kuna vyeo ama afisi zingine ceremonial. Kwa mfano afisi ya Assistant Chief, afisi ya D.O tunasema ni ceremonial. Tuwe na afisi moja pale kwa grassroot - afisi ya Chief, halafu baadaye tuwe na afisi ya DC: Hizo mbili nafikiri zimetosha kwa grassroot. Hata provincial office tunasema ni ceremonial. Na pia, tunasema ya kwamba yule ambaye anachaguliwa kama Chief kwa grassroot, awe ni mtu ambaye ana masomo zaidi ya kidato cha nne.

Sehemu nyingine ambayo niko nayo ni Local Government. Kwa Local Government ili mtu awe civic leader lazima mtu huyo awe ni mtu ambayeamesoma vya kutosha, aweze kuchaguliwa na wananchi na awe amesoma hadi kidato cha nne.

Pia, na ile kufanyiwa interview ili kujua kama anajua Kingereza ama - hapana ama Kiswahili, ikiwa ana masomo ya form 4 awe amepita Kingereza na pia Kiswahili - mtu ambaye anaweza kuongea kwa watu. Tuna suggest pia wale Mayors wa Councils na Machairmen wawe elected na watu na waweze kuserve kwa term ya miaka mitano si miaka miwili tu.

Katika Parliament, pia tunasema yule mtu anataka kuwa Parliamentarian anahitaji kuwa mtu amesoma na awe na miaka zaidi ya 30, mtu ambaye amekomaa. Na tumegundua kwamba mtu akiasha anza kuwa mzee yaani zaidi ya miaka 70 - tunataka kuwe na limit - MP awe between 30 – 70 years, maximum. Watu wakiwa zaidi ya miaka sabini, wawe wamejitayarisha kufanya kazi zingine.

Katika afisi ya Rais, tunasema mamlaka ya Executive ni mengi sana ambayo yako vested in that office: Kwa hivyo, kama inaweza kupunguzwa: Kwa mfano, uteuzi wa afisi zingine kama P.S, afisi za Directors ama Civil servants wengine, badala ya President kuchagua kuwe na uwasiliano kati ya Bunge na kamati ambayo inaweza kuundwa ili iweze kuteua maafisa hao.

Pia nataka kusema kwa upande wa natural resources. Tunasema kwamba natural resources zetu ambazo ziko nchini Kenya ziweze kuwa managed na Wananchi wa sehemu hiyo. Kwa mfano, forest sehemu hii iweze kuwa ni ya watu wa Lugari. Kukiwa kuna faida ya aina yoyote ile, iweze kufaidi watu wanaokaa upande huo.

Land ownership: Kila Mkenya aweze kukubaliwa kuwa na shamba mahali popote. Nakubaliana na yule aliyezunjumza kwanza kwamba, land ownership iwe restricted to a maximum of 50 acres, - siyo zaidi ya hiyo.

Pia, tunasema wasichana wetu na wavulana wetu, should be equally allowed to inherit land from their parents: na pia, women should be involved in land issues kwa mfano, land title deeds wazee wakubali ziandikwe katika majina mawili kama mlipata na mama - ya mama na ya baba.

Upande wa Judiciary, there should be Constitutional rights to legal aid kwa case zozote zile - sio tu tuwe na wengine wanawakilishwa lakini - kama mtu amefanya kosa aweze kuwa na mtu wa kumwakilisha.

Nikiendelea kumaliza, kuna sehemu ya worship: Ingawa tuna freedom of worship, lazima ichunguzwe sana kwa sababu, katika sheria ya Kenya tuweze kuworship Mungu mmoja, kwa sababu kuna wale wanaworship mungu mwingine. Nafikiri sheria iweze kusema ni Mungu wa aina gani watu wanatakiwa kuworship, na awe ni yule mmoja tunayejua. Registration of churches kwa upande wa worship, tunasuggest ya kwamba regitrer of societies kuregister makanisa awe na special committee ya spiritual leaders who can determine genuine churches.

Com. Aroni: Thank you very much, but we need to clarify one or two things with you.

Com.Ratanya: Okay, Bwana Simon, kuna maswali kama mawili ya kufafanua tu. Pengine una memorandum yako utatupatia. Ya kwanza ni mambo ya provincial adminsitration. Umesema afisi zingine ni ceremonial - lakini hapo ningetaka ufafanue vizuri kwa sababu hapa hukueleza vizuri kuhusu ya machief, D.C Assistant Chief, D.O P.C – wale ungetaka waondoke ndio ceremonial, ufafanue vizuri. Kwa sababu kwa record yangu D.O, Assistant Chief na P.C. ni ceremonial - those ones should go. You clarify that. The other one, umesema elimu ya Councilor iwe ni ya form 4, lakini sikusikia kama ulifafanua vizuri qualification ya MP na hata ya President, pamoja na umri wa President, minimum na maximum upeane zote kwa sababu ulikuwa ukienda kwa haraka.

Mr. Simon: Provincial Administration tunasema - nitazungumza hapo kwa Kingereza kwa sababu nimeandika kwa Kingereza. The current structure should be trimmed to avoid duplication of the duties and some of those offices are ceremonial. For example, the office of the Assistant Chief and the office of the Chief. Hizi ofisi mbili zinafanya karibu kazi moja. Pili, ili jambo lolote litambuliwe katika afisi ya DC, lazima kuwe na hizi signatures mbili. Sasa tunajuliza kwa nini. Si tuwe na signature moja tu ambayo inaweza kucover sehemu hiyo yote? Na utapata ya kwamba, most of the locations zile tunazo sasa kuna either Assistant Chiefs wawili ama watatu. Na utapata kazi nyingi inafanywa na Chief - sio na Assistant Chief. Kwa hivyo tunaona pengine yule Chief anaweza kushikilia ile kazi ya Assistant Chiefs afanye zote.

Kwa grassroot kabisa tulikuwa tunapropose tuwe na yale tunaita “Likuru”, yaani wazee wa mitaa ambao wana masomo, wale ambao wakifanya kitu kwa kijiji, hiyo inapitishwa tu hodi kwa afisi ya Chief.

Na maCommissioners, mtanikubalia kwamba nikisema hivi, kwamba sisemi wale ambao wako sasa, yaani kama Assistant Chief wangu, asifikiri ninasema aende kesho. Iwe gradual phase - out, iende polepole, yaani wanapofika retirement waende. Kama kuna afisi inaweza kupotikana kwa afisiya D.C, wale ambao wako sasa wapewe kazi hizo.

Afisi ya D.O pia ningependa kuclarify. Mara nyingi kwa afisi za D.O, kazi nyingi inayofanywa, inafaywa either na chief ama na

D.C. Kwa hivyo, hata D.O anapokupa signature aina yoyote ile, ni lazima kuwe kuna signature ya Chief na pia ya D.C - ndio ikubalike. Kwa mfano kwa Lands na kadhalika. Ndio sababu nilikuwa nasema hivyo. Afisi nyingine ile nimetaja ni ya P.C. Mara nyingi kazi nyingi zinamalizikia kwa afisi ya D.C. Kwa hivyo, tunapropose kuwe na afisi ya D.C badala ya ile ya P.C. Kwa Upande wa swali la pili, kwa upande wa Mbunge, awe na miaka kati ya 30 – 65.

President tunapropose miaka 40. Mtu ambaye amekomaa. Pia, asipite miaka sabini kama vile ambavyo nimesema kwa Mbunge. Hata zile electoral positions zote ziwe zina hiyo limitation ya miaka ili mtu aweze kuhudumia watu wakati bado ana ile nguvu, kama bado yuko dynamic kufanya ile kazi. Akishafika miaka 70 - nawaheshimu wale wazee wa miaka 70 lakini, akishafika miaka 70 basi aweze kufanya kazi zingine, siyo kazi ya kurepresent tu wananchi.

Com.Aroni: Ahsante sana, tafadhali jilandikishe na kutuachia hiyo karatasi. Kanuti Imbuka.

Mr. Kanuti: Chairman na wananchi wote mnakaribishwa. Hamjambo? Haya ndio maoni yangu: kama kuna kuchaguliwa kwa Minister naitwa Kanuti Imbuka. Minister wateuliwe kutoka kwa Wabunge ambao wamechaguliwa kupitia kura - sio wale wako nominated. Na kama kuna extension yoyote, watolewe kwa Permanent Secretaries.

Sehemu ya pili, naona hii 2 term period ya President iwe extended pia hata kwa Wabunge. Mbunge asizidishe terms za office mbili. Iende hata kwa MaCouncilor na sehemu zote ambazo zinapigiwa kura. Hata BOGS na makundi mengine. Halafu, Katiba iwe na sehemu ya kuturuhusu sisi wapiga kura kumtoa Mbunge ambaye hatutumikii kama vile tunavyotaka.

Halafu sehemu zingine ambazo mimi naona zinatatiza ni mabaki ya sheria za kikoloni. Minority ama wachache ambao tunapoenda kukaa kwa upande wa kienyeji tunasumbiliwa sana, kufuatiliwa na bunduki kwa pombe kienyeji - mkebe mkebe hivi. Tunaona tunateseka hapo. Ninataka Katiba itulinde. Tusilazimishwe kunywa tu pombe za watu wengine na zetu za kienyeji zitupiliwe mbali - zisiitwe zote ni haramu.

Sehemu ingine. Kwa vile inaonekana ni business, tupewe permit za kuweza kuunda kama unataka kuuza. Lakini ya matumizi pia turusiwe tuweze kutumia bila kufuatafuata kila mahali.

Halafu ikiwezaekana, party ambazo ziko saa hii ni zile za waanzilishi. Kwa hivyo mtu mwingine akijitokeza akitaka kuingia anafungiwa nje. Ninataka Katiba iruhusu mtu ambaye anasupport, kusimama kwa uchaguzi hata bila kuwa mwanachama wa party yoyote.

Halafu vyama navyo vimekuwa vingi sana. Vile vizito vine vya kwanza vihifadhiliwe na vile vingine viachwe. Otherwise vitaanziswa vingi kwa sababu vitakuwa kama ni mapato au biashara kwa watu kwa hivyo vyama vine tu ambavyo vina uzito wa

watu viweze kufadhiliwa na vingine vijitegemee.

Halafu, mambo ya mapato. Inaonekana kama wananchi wa Kenya wengine wanilipwa zaidi kuliko wengine. Mimi naona kama kungekuwa na Kamati moja ambayo inasimamia mishahara ya wananchi wote, na mishahara hiyo iwe ya kipimo kutoshana na mapato ya nchi. Isiwe wengine wanapata mamilioni na wengine wanapata makumi. Hii inaonekana hata kwa saa hii. Halafu tuje kwa sehemu ingine - hicho kikundi kiwe na wanachama kutoka makundi ya Labour organizations, Professional, unions na hata madaktari: Kwa sababu tunaona Wabunge wanajichagulia mishahara. Hata wanapangia maprofessors mishahara na hao Wabunge ni watu ambao ni mtu yeyote anaweza kuwa ni mtu ambaye amefanikiwa kutoboa kura na akaingia kwa Bunge.

Halafu sehemu ingine, naona kuna sehemu ambazo zinapitishwa kwa Bunge na zinawawacha wananchi wengine kando. Mimi naona kama pension system ya Wabunge kuweza kupata pension baada ya kufanya miaka 10, iwe extended kwa Wakenya wote. Ukifanya miaka kumi hata kama ni Chief, ukitoka hapo uwe na haki ya kupata pension.

Halafu sehemu ingine ambayo mimi naona ni ya kura. Tukibebana na hii mikebe ya kura kwenda kuhesabu kwa Central Counting Station kuna ujanja mwingi sana. Zihesabiwe katika voting station.

Halafu Ministry ya Labour. Tangu mimi ni one, thini imekuwa ministry ya kupinga migomo- haina clear policy. Mimi naona hiyo Ministry itolewe, kuanzishwa Ministry of Human Resources and Employment yenye itajali masilahi ya wafanyikazi wa Kenya. Ministry of Labour inatetea tu employers. Hata kama wale wanataka kugoma wana haki, Ministry of Labour inakanyagia tu chini. So, employers huwa wana haki ya kuweza kuwafanya wafanyikazi wao watumwa.

Com.Aroni: Please summarize.

Mr. Makuti: Yes. Then kuna sehemu ingine madam, ambayo ninaona kuna Private armies ambao wameanza kumea wakiruhusiwa, nashindwa kama tutakuwa na nchi ya kutunza. Hiyo kitu itolewe kwa Katiba. Sheria iheshimiwe na kila mwananchi hata kama ni President.

Halafu Treasury ya nchi iwe moja-kusiwe na Treasury moja kwa Office of the President, ingine kwa State House, ingine kwa individuals.

Mwisho, naona kama double-cheque system itolewe kwa kila mwananchi. Maadvocate wamekula pesa za insurance za wananchi nyingi sana. Wanapata kama maybe mia nane elfu, wanapatia mtu kama 30,000/= zingine wanaficha kwa sababu huyo mtu hajui kuwa amelipwa nini labda tuseme ni malipo ya accident.

Then, ikiwezekana, Party founders wasikubaliwe kuwa the owners of Parties.

Com.Aroni: Thank you very much.

Mr. Kanuti: Nimeshukuru hapa ahsante.

Com. Aroni: Ahsante. Jiandikishe na utuachie karatasi - Bi Margaret Wanyonyi.

Esther: Thank you very much. I am not Margaret Wanyonyi, I am Esther Werangai.

Com.Aroni: In our list, we have Margaret Wanyonyi. If we have Margaret Wanyonyi let her come and we will get to you. Lugari Maendeleo ya Wanawake -Margaret Wanyonyi. Kama hayuko, ahsante sana-. mama tutafikia jina lako. Sammy Kwea. Is Margaret Wanyonyi there, akifika anyway, atatueleza tuone kama tutampatia nafasi.

Mr. Kwea: Ahsante sana, Chairperson Abida Ali Aroni. Mimi kwa majina najulikana kama Sammy Kwea. Hapa mbele yenu nimebeba memorandum inayowakilisha Kikundi cha Wakulima kutoka Lugari Division. Katika hii memorandum yetu, tumeongea kwa mambo yafuatayo: Tumeongea juu ya Executive, Land property rights, Environment and natural resources and Local Authority pia bila kusahau, tumeongea kitu kuhusu Men's rights.

Nafikiri nikifanya summary kuhusu Executive, ni maoni yetu kwamba President wa nchi ya Kenya atumike vipindi viwili vya miaka mitano kila muhula. Ikiwezekana, uwezo wa President uweze kurudishwa chini kidogo kuliko vile ulivyo sasa kwa sababu, huo uwezo mwingi umelete utumizi mbaya kwa hiyo afisi ya Rais. Pia, tumeonelea kwamba President asiwe above the law, sababu akiwa above the law atatumia hiyo afisi vibaya na kuwa na abuse of office.

Kuhusu Provincial Administration tulikuwa tumeonelea ya kwamba Chiefs and Assistant Chiefs ni Civil servants; wana hitaji kuwa na transfer kama Civil servants wengine. Ili tusiwe na mahali ambapo kuna Chief ambaye hawezi kuwa na matunda mema katika hiyo location, nitabaki tu namna hiyo. Nafikiri akiwa transferred anaweza jaribiwa mahali pengine tuone kama anaweza kufanya kazi vizuri huko kuliko tu kuwa pahali moja. Ikiwa mtalala hivyo mnalala hivyo miaka yote thelathini mkiwa naye.

Kuhusu afisi ya Vice President, tumeonelea ya kwamba VP asiwe anateuliwa na Rais vile inafanyika sasa maanake, unaweza kupata kwa kipindi kimoja, kuna VPs karibu watano. Kwa hivyo ni maoni yetu ya kwamba, political parties wakati zinapo nominate Presidential candidates, ziweze kuname running mate- ambaye atakuwa automatic VP katika hicho kipindi chote cha miaka mitano. Kwa hivyo haina haja apigiwe kura yeye kwa sababu President wake akishinda, he is automatically the VP.

Na ikiwezekana, hicho cheo cha VP kitolewe tuwe na Deputy President ambaye anaweza kuact kama President wakati

ambapo President ako nje kwa shughuli zingine za kiserikari. Sio kama sasa, tangu tuwe na independence we have never had an acting President.

Upande wa land and property rights, tungependa land property iangaliwe. Land ownership imekuwa abused. Unakuta kuna mtu ako na acre arobaini ya shamba na ambapo mwananchi mtukufu mwingine wa Kenya hana hata mahali pa kuzika panya wake akifa. Kwa hivyo tungalipenda tuwe na viwango viwili vya land ownership. Kuna wale large scale farmers. Hawa wanaweza kuruhusiwa wawe na zaidi ya 200 acres. Mwananchi wa kawaida, isizidi 50 acres ili wananchi wengine pia nao waweze kupata mahali pa kukaa na kuishi. Pia, katika hiyo land, sisi kama wakulima tumeona, ukiangalia katika Katiba yote utaona hakuna mahali ambapo tuna Food Policy. Na kama Wakenya tunajua, uwe unalima au hulimi, ni lazima ule. Kwa hivyo, wale wanaolima, tungependa tuwe na kifungu kwa Katiba ambacho kinajali maslahi yetu na kuhakikisha kwamba all agricultural inputs ziwe subsidized by the Government ili tuwe na chakula cha kutosha kutulisha sisi, na wale wenye hawalimi.

Katika upande wa mazingira, yametumiwa vibaya sana kiasi ya kwamba, hata wakati huu hapa tunaposimama Lugari huu ni wakati wa mvua ya masika na hatuna mvua hata mkiona mashamba yetu. Na hii ni kutokana na matumishi mabaya ya mazingira. Tunakata forests zetu bila mpango. Ukienda hapa juu, shamba la Tani ilitumiwa vibaya, ilikatwa bila kuuliza wenyeji na sasa ime-cause sisi kukosa mvua. Kwa hivyo tungehitaji-katika afisi ya DC, kuna D.O wa environment na hakuna kazi anafanya kuangalia hiyo environment. Watu wanaharibu water catchment areas, wanakata miti huko and nobody is stopping them. Kwa wanaolima katika miinuko ya mitoni, pia waangaliwe ili tujue vile tunakuwa.

Nikirudi kwa upande wa Local Authority tulikuwa tumegusia kuwa mtu yeyote kuwa Diwani, ni lazima awe na elimu ni kiwango cha chini kabisa cha kuwa form 4, mwenye amepata alama ya D+ and above. Wao pia wapewe muda wa kuhudumu katika afisi ili wasikae huko wakasahau, wakafikiria kuwa ni mali yao. Chairman or Mayor wachaguliwe direct na watu. Council, vile mlikuwa mmeuliza, yenyewe igenerate pesa ile italipa Councilors mishahara yao. Tukiwa na Board ambayo itasimamia mapato ya Council, hiyo inaweza determine mishahara ya Councilors.

Nafikiri pia tulikuwa tumeonelea, we can still maintain nominated Councilors kwa sababu kuna mambo maalum wanafanya. So, kwa kifupi, hiyo ndiyo memorandum yangu.

Com. Aroni: Asante. Tafadhali jiandikishe. Tom Lyambila – KNUT Lugari.

Mr. Lyambila: I am Lyambila, the executive Secretary KNUT Lugari branch, presenting a memo on behalf of the teachers in this district.

Dear Commissioners, the branch on behalf of the teachers in this district, recommends the following: There should be a preamble in the Constitution which shows the unity of Kenya. It should also reflect where we came from as fragmented tribes,

where we are going- towards one people of this nation with a common language.

We have looked at different issues raised by your questionnaire but because of time, I may not go through all of them. One, directive principles of State policy: we, in Lugari as teachers feel that the Constitution should have brief statements capturing the philosophies of this country, for example Harambee. Democratic principles are vital in the Constitution and hence, they should be enacted in spelling out all human rights. Kenyans have important values such as cultural values that should be reflected in that Constitution.

We feel that, in the new Constitution to be written, there should be no use of the word “tribe”. Instead there should be, “the people of Coast”, “the people of Nyanza, “the people of the Rift Valley”.

On Constitutional supremacy, we feel that we should retain the Parliamentary powers to amend the Constitution by 65% majority vote. The powers of Parliament to amend the Constitution should be limited. E.g. on certain crops in Kenya. People growing that particular crop should be consulted before Parliament amends the laws governing the sale or marketing of that crop.

On citizenship, we feel that an automatic citizen is a Kenyan whose parents are both Kenyan. But we feel that Kenyan citizenship can be acquired by one who is born of a non Kenyan parent and they declare in court that they agree to be Kenyans. Hence, they can be registered as Kenyans and that non-Kenyan parent should also be registered. A Kenyan citizen has the duty to safeguard the country for his existence.

Ladies and gentlemen, on security and defense, we had the following to recommend; that, the Constitution should enhance for the discipline of the armed forces. The current laws should apply. But for their welfare, a Council should be formed to cater for the forces complaints and also their salaries. The Republic President remains Commander-in-Chief of Armed Forces Constitutionally. We recommend that the powers to declare war and permission to use extra-ordinary powers be vested in Parliament and not the President.

On political parties, we recommend that the Constitution should allow multipartyism but only --- line for a political party to be registered, it must also in addition to the 3000 people, atleast 10% be from each province of Kenya and whose ½ must be women. The Treasury should fund political parties, since the cash is from the tax payers who are owners of the party. Such funds be subject to audit by the Auditor General. The funding should be limited to 3% of the national budget.

Structure and systems of government; we are recommending that the unitary system of government remains because it is easier for Parliament to monitor such a government.

On legislature, Parliament should vet all proposals given by the President and not the President to veto the Parliament's procedures. The President is only to be Chief Executive Officer of the Kenya government and is to be vetted by Parliament. I have written here a few functions – you will read through, of what should be done by the President and the legislative Council. They are many.

I now go to the Executive. The Constitution must specify qualification for a Presidential candidates. For example, he/she must have attained form 4 level of education, must be mentally healthy, ethically and morally fit. He must declare his wealth before he becomes President. The tenure of President be 2 terms of 5 years whose functions are defined by the Constitution. For example he remains Commander in Chief of the Armed forces e.t.c. The President may be removed from office through impeachment or referendum.

On the Judiciary, we are recommending that the Constitution should allow village courts where simple matters can be heard. There cases are such as those of encroachment on one's land through alteration of boundary. There should be a Constitutional court appointed by Parliament and recommended by the LSK whose members should have a law degree from any university at both levels- that is at the Constitutional court level as well as village courts.

The Local Government, we are recommending that Mayors and Council Chairmen be subject to election directly by the people. They will serve within the Municipality or the Council. The Kenya Constitution should specify that any person to hold office be ethically, morally and mentally stable and at least a form 4. Mayors and Council Chairmen be in office for 3 years before another election.

In Kenya we want to suggest that Ministers be vested with powers to dissolve a Council if in his view, the Council has failed to deliver- once he receives 1000 signatures of the complainants of that area.

The electoral system and process; we are recommending that the present system remains. There should be simple majority rule at both Local authority and Parliament and women must form 1/3 of the composition.

Defecting and switching of political parties should not be allowed in the Constitution. But a person who defects or switches, should sit back on the bench and a new person vies for that seat.

Com. Aroni: Please summarize now.

Mr. Lyambira: Okay. For one to be declared a winner, at least one should have 25% of all the votes from the registered area. Parliament should have 300 seats and also we are recommending that six seats be reserved for these bodies; Trade unions two, farmers one, traders one, youth one and disabled one.

Because of time Commissioners, on the basic rights I will only say one thing. It should be in the Constitution that the government should ensure water, security, health care, shelter, food and employment as basic rights for all Kenyans. The government should levy all Kenyans to fund education.

On land ownership we are suggesting specifically how much land each person should have in Kenya. It should not go beyond 50 acres for an individual, and whose 10% should be under trees. Thank you.

Com. Aroni: Thank you very much. We shall read the rest. I gave you more time because you are representing teachers and we know they are important people. But I cannot now go beyond the time that I gave you. Ron Luvai.

Mr. Luvai: Ahsante Madam Clair. Majina yangu ni Ron Luvai. Nitawasomea memorandum yangu. "The Constitution of Kenya should have the following. All governmental ministries should be created by Parliament or the Head of Civil Service in consultation with Parliament and not the President as is the case currently. All government Ministers should be appointed by the President as is now but, only in consultation with Parliament. The same for Permanent Secretaries.

Landless people should be resettled as this was one of the objectives of freedom. This will reduce poverty and bring equality. It is the duty of Parliament to accomplish this.

Corruption should be gazetted as a sin and whoever commits it must be prosecuted as per the Constitution.

The Judiciary as the arm of law should be independent. It should be.....(elevated to the office of by the approval of Parliament.

Defense. The power of defense should be controlled by Parliament as opposed to the present where the Head of State is also the Commander -in-Chief of the Armed Forces. It is the role of Parliament therefore to call a state of emergency, as opposed to the current position. The political appointments should be done with the approval of Parliament in consultation with the Head of Civil Service.

The new Constitution should include the post of PM who will also be Kenya's foreign affairs spokes person, as opposed to the present where the Foreign Affairs minister is the spokesperson of Kenya's policies.

Resources: this is a national cake so it should be shared equally nation-wide. For example National parks and game parks should be spread nation-wide so that all nationals benefit. Thanks.

Com. Aroni: Thank you very much for keeping time. Tafadhali jandikishe pale. Next we have Nicholas Shiuka.

Mr. Shiuka: My name is Nicholas Shiuka. The System of government that I would like us to have is a federal government with eight Provinces in Kenya.

Also, we need a PM in our government who should be the Head of the State. On the side of President, he should remain ceremonial and as a unifying figure.

On the side of elections, the President should attain 50% votes also should his runny mate. In the absence of this 50% votes, the political parties should form a Coalition Government.

Changing the Constitution should be done through referendum.

We also want a President without a constituency- somebody to be picked and if he is popular he contests and becomes the President.

The President should not be above the law. During elections, the Speaker of the National Assembly should act as the Head of Government not that the President is still the head even as the elections are going on. No.

Legislature, Executive and Judiciary should respect one another. Sometimes, you find that the Executive is interfering with the Judiciary.

We also want a government that equitably shares out powers regardless of political affiliation. We should give the Parliament more powers even to select the Heads of parastatals.

If the electorate reject you, you go back home and relax. Not the way it is now, that you failed elections and you get appointed. I think that is all that I had.

Com. Aroni: There is one clarification.

Com. Ratanya: Mr. Nicholas, there is one clarification. You have mentioned that we should have one PM. It is not very clear whether you are saying the PM should be Head of State or Head of Government. Can you clarify that?

Mr. Shiuka: Head of Government.

Com. Ratanya: Thank you.

Com. Aroni: Thank you. Please register. Next is Tabitha Nguhe.

Ms. Nguhe: Majina yangu ni Tabitha Nguhe. Commissioner na wananchi wote nawasalimia.

Hapa nina maoni machache. Maoni yangu ni juu ya elimu. Naona kwamba, elimu ya shule ya msingi iwe ya bure na tena iwe ya lazima kwa kiwango fulani kwa sababu tunapata kuwa kuna umaskini sana ndani ya jamii zetu na unapata kuwa imekuwa mzigo sana hata kusomesha watoto especially kwa watu ambao wamekuwa settlers juzi, wale wamekuwa hawana mashamba, wawamepata hivi majuzi. Tunapata kuwa hawa watu wana shida sana. Hata mzazi hawezi kupata pesa ya kusomesha huyu mtoto hata class one or two. Unapata mtoto huyo yuko tu nyumbani na ukiuliza mzazi anasema hana pesa.

Unapata kuwa serikali haingilii. Huyu mtu anayeshughulika. Huyu mtoto iwapo hatasoma, kutakuwa na shida sana kwa ulimwengu wa sasa, kwa mtu ambaye hajui kusoma.

Katika system ya education, naona ibadilishwe kutoka 8:4:4 irudishwe kwa 7:6:3 ili kwamba mtu anapomaliza form 6, anakuwa na uhakikisho wa kupata kazi hata ingawa hajafika university.

Katika upande wa waalimu, naonelea waalimu wawe distributed equally. Kusiwe na shule zingine ambazo waalimu ni wengi, na ukienda kwa shule zingine waalim ni wachache. Hii husababisha shule zingine kufanya vizuri ni zingine hazifanyi vizuri na hii ni kwa sababu shule pengine imepewa walimu wachache au labda walimu ambau hawajafuzu vizuri Katika discipline kwa waalimu, naona iwe inatekelezwa. Waalimu wachukuliwe hatua ikiwa watafanya mambo yasiyofaa, kama kuwatesa wanafunzi, au iwapo watafanya mapenzi na wanafunzi. Wachukuliwe hatua, hata ikiwezekana, katika hiyo hali, mwalimu afutwe kazi.

Katika ile punishment kwa wanafunzi, naona kwamba, kupigwa viboko iondolewe. Na sio kwamba huyu mwanafunzi asiwe punished, bali kwamba kuwe na aina nyingine ya punishment ambayo watu watajadiliana na waone. Lakini, nilionelea kuwe na aina nyingine ya punishment sio kiboko. Punishment ambayo mwanafunzi atapewa ajisikie amechoka ama a regret.

Katika afya zetu, ningenelea kwamba kuwa na suitable facilities in all health centres, ili wagonjwa waweze kuhudumiwa vizuri. Tunapata kuwa unaweza enda kwa health centre fulani unaambaiwa pengine hakuna vitu fulani, na unapata kwa health centre fulani hizo vitu ziko. Hizo ziwe distributed vizuri na kuhakikishiwa kwamba kila hospitali iko nazo.

Naona kwamba wale madaktari na wale wasimamizi wa madaktari wasiwe na private clinics kwa sababu hizi zinafanya kwamba madawa yanaibiwa kwa mahospitali na zinapelekwa kwa hizo ma clinic. Ukienda hospitali unaambiwa hakuna madawa na unakuta huyo daktari anakwandikia uende kwa clinic fulani ambayo ni yake ukienda huko, unaenda kununua madawa. Kwa hivyo ninaonela kwamba hizi private clinics kwa madaktari ama wasimamizi wa madaktari ziondolewe.

Pia, kuwe na free medical services kwa health centres. Lakini iwapo mgonjwa atakuwa admitted, hapo ajisimamie mwenyewe.

Kwa sababu unapata kuwa watu wana shida nyingi na pengine mtu ni mgonjwa nyumbani, na hana pesa ya kwenda hospitali anaumia tu, kwa sababu akienda hospitali anaitishwa pesa ambazo hawezi kugharamia na huyu mtu anaweza kufa kwa ugonjwa kwa sababu hana msaada wowote. Akiangalia huku, hana chochote. Naomba kwamba serikali iwasaidie, ili kuwe na kutibiwa bure kwa kiwango fulani. Lakini ikiwa ni zaidi, mtu ajisimamie. Ni hayo tu.

Com. Aroni: Ahsante sana. Jiandikishe tafadhali. Michael Munde.

Mr. Munde: Nawasalimu nyote, hamjamboni? Mimi kwa majina naitwa Michael Munde na niko na maoni machache hapa.

Ninaanza na natural resources. Ninaonelea hivi; katika Katiba kuwe na sheria ambayo inasema kuwa watuchukulie natural resource kama forests. Forests ziwe na manufaa kwa watu ambao wapo kwa eneo hilo. Kwa mfano tunaona kuwa kuna forests nyingi ambazo zimekatwa huku lakini watu ambao wako katika eneo hilo hata kuni peke yake hawaruhusiwi kuchukua. Ukichukua kuni unashtakiwa. Pia, forest ile ikikatwa, kuwe na mit mingine ambayo ishapandwa, inaanza kumea, ili wakati hii ikitoka, ile ingine pia inaendelea kukua.

Upane wa kupiga kura: Kupiga kura kuwe lazima kwa kila mtu kwa sababu serikali hutumia pesa nyingi sana kutengeneza vitu vya kupigia kura kama vile kadi za kupiga kura. Inatumia pesa hizi ambazo zingetumika kwa kazi nyingine tofauti. Ili kila mtu apige kura, siku hii iwe National Day kusiwe kazi inafanyika-watu wote waende kupiga kura.

Halafu, katika upande wa kupatiana kadi za kupiga kura, ziwe zikipeanwa wakati ule vitambulisho vinapeanwa pia wakati mtu anajiandikisha hupewa kitambulisho, pia anajaza kadi ya kura vilevile.

Shelter: wakati squatters wanapewa mashamba, ni vyema kama serikali ingewasaidia kuwajengea hata nyumba kwa sababu ukiangalia squatters, wengi wao nyumba zile wanaishi ni nyumba ambazo ukizona. Wangesaidiwa kujengewa hizo nyumba na hata barabara - wengine hata hawawezi wakafika kwao kwa sababu barabara hawana. Ni hayo tu.

Com. Aroni: Asante. Jiandikishe tafadhali. Daniel Osiru Ochomo.

Mr. Ochomo: Kwa majina ni Daniel Osiru Ochomo kutoka pale Mautuma, Makutano market.

Aina na ***** serikali: Maoni yangu binafsi; Nitaogea Kiingereza na pia natachanganya kiwahili. From records of the revised edition (1998) Laws of Kenya printed and published by Government printer Nairobi, a book of Laws of Kenya Constitution, I select a system of government different from the current one whereby chapter 2; executive- part 1 section 14, 1

& 2 .

Protection of President in respect to legal proceedings during his term in office. I am against this chapter. Part 2 Section 14, I and II.

We should have majimbo and also establish *ufalme* in which our 42 tribes each appoint its king as was practised before independence by our grandparents and clan members.

Federal government has to replace the Presidential government.

In Legislature, I prefer in our next government, MPs to expand their functions. Age limit remains. Language tests should increase from current two to three vernacular or language spoken by people of one area. One Parliament to be for government and another on of our chosen tribe leaders to discuss taboos related to our own people.

Land and property rights: Local government should have ultimate power over it and will be released to the family of the deceased who will hand it down to children and grandchildren.

Succession and transfer of power: The Speaker should be incharge of Executive powers during Presidential elections. Presidential results should be declared at the polling station and for tribal leaders, should be conveyed through the media e.g. television, newspapers, radio e.t.c.

Cultural, ethnic, regional diversity and communal rights. *Kwa upande huu, naonelea hivi*: I assume every tribe has men who possess spiritual powers suits women. These should be distinguishing and their interests be catered for in the Constitution. Their interests should be catered for in the Constitution.

International relations: *katika serikali ya federal au majimbo*, the government's foreign affairs be the responsibility of the Executive. For the boundaries, tribal leaders should be responsible.

Participatory government: *kwa federal government, majimbo iruhusu NGOs and other groups in governance*. As such every province to have several NGOs.

Lugari district should be given a Law Court, tarmacked roads and NGOs. This should be considered also for other distircts like Lodwar, Turkana, e.t.c.

Judiciary: In the majimbo government, Parliament to be given more powers to appoint ***** judges in conjunction with Judicial Service Commission rather than the President only as is in the current situation.

